**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **Ijumaa, 02nd May 2003 Asubuhi**

---

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).

2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.

3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali lina alama nne (4).

1. (a) Toa maana ya kitenzi kishirikishi na toa mifano miwili

   (b) Eleza tofauti kati ya kitenzi kishirikishi na kitenzi kauli kwa kutumia sentensi

2. Fafanua maana ya muktadha wa kifasihi na eleza aina nne za muktadha zinazoweza kutumika katika kazi ya fasihi

3. Chunguza maneno yafuatayo kisha ueleze aina ya vivumishi vilivyotumika na maana yake katika sentensi:

   (a) Vijana wote walishiriki shindano

   (b) Alipanda miti kumi

   (c) Wanafunzi hao walikumbatia mabadiliko

   (d) Alinunua gari jekundu

4. Kwa kutumia hoja nne, eleza umuhimu wa kutumia mashairi ya Kiswahili katika kukuza uwezo wa lugha miongoni mwa wanafunzi wa sekondari

5. Fafanua dhima ya kazi ya hadithi fupi katika kukuza stadi za kusikiliza, kuelewa na kueleza kwa wanafunzi wa sekondari

6. Bainisha hatua nne za maandalizi ya vipindi vya lugha ya Kiswahili kwa kutumia mbinu shirikishi

7. Eleza tofauti kati ya majukumu ya mwalimu na wanafunzi katika utekelezaji wa mbinu za ujifunzaji unaomwelekeza mwanafunzi

8. Jadili kwa kifupi athari za kutumia mbinu ya mihadhara pekee katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa sekondari

9. Kwa kutumia mifano, taja aina nne za sentensi za Kiswahili na eleza muundo wa kila moja

10. Tunga sentensi moja kwa kila aina ya kielezi kifuatacho:

    (a) Kielezi cha namna

    (b) Kielezi cha kiasi

    (c) Kielezi cha wakati

    (d) Kielezi cha mahali



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

11. Andika insha ya hoja inayoeleza mchango wa lugha ya Kiswahili katika kuendeleza sekta ya elimu nchini Tanzania

12. Kwa kutumia hoja tano, jadili sifa muhimu za mhusika mkuu katika kazi ya tamthilia ya Kiswahili

13. Eleza hatua sita za kufundisha kipengele cha matamshi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

14. Tathmini tofauti kati ya lugha ya fasihi na lugha ya kawaida kwa kutumia hoja sita

15. Eleza changamoto zinazowakabili walimu wa Kiswahili katika kutekeleza mitaala ya umahiri kwa shule za sekondari za umma

16. Kwa kutumia hoja tatu chanya na tatu hasi, eleza athari za matumizi ya mchanganyiko wa lugha (Kiswahili na Kiingereza) miongoni mwa vijana wa sekondari nchini Tanzania


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org